



SIKU 16 ZA UANAHAARAKATI 2023

MSHIKAMANO! UWEKEZAJI! HATUA THABITI!

MWONGOZO WA SHUGHULI ZA VYOMBO VYA HABARI

Tumeshuhudia kupungua kwa kiasi kikubwa nafasi za kutetea mabadiliko ya kijamii ya kifeministi, kuhakikisha usalama, na utokomezaji wa Ukatili Dhidi ya Wanawake, tunakualika ujiunge na Mshikamano kwa Vitendo ili kuangazia hali hiyo na kutoa wito wa kuchukua hatua thabiti.

Mwongozo wa Shughuli ya Vyombo vya Habari unawakilisha baadhi ya hatua ambazo unaweza kuzingatia katika kampeni yako.

1. Mitandao ya Kijamii

Mitandao wa Kuzuia UWAKI, unatarajia kuzindua kampeni ya mitandao ya kijamii katika Siku 16 za Uharakati ili kuwahamasisha wanachama na jamii zetu kuwa na mshikamano dhidi ya tishio linaloendelea dhidi ya haki za wanawake, na kutoa wito kwa wafadhili kuwekeza zaidi na kwa ubora katika shughuli za kuzuia Ukatili Dhidi ya Wanawake. Katika mwaka huu wa 2023, tutazingatia zaidi katika kujenga Mshikamano wa Kifeministi na kuwekeza kikamilifu katika kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake.

Tutatumia majukwaa yetu ya mitandao ya kijamii, Twitter, Facebook, Instagram, na WhatsApp kutuunganisha, kuwa na umoja na kuzingatia maadili yetu ya pamoja ya undugu na kanuni zetu za kifeministi. Jiunge na mazungumzo ya kikanda. Wakati wa kampeni, pia tutashirikishana vibonzo vya Kampeni za Mitandao ya Kijamii ambavyo shirika lako linaweza kushirikisha moja kwa moja kwenye mitandao yako. Kumbuka kutumia hashtag hizo hapo chini kujiunga kuifanya kampeni iwe na mwitikio mkubwa.



#16DaysOfActivism

#SolidarityActionInvestment

#SolidarityInvestmentAction

Fikiria wakati ambao ulipata usaidizi wa kifeministi wakati ukiwa na changamoto. Shirikisha hadithi yako na tafakari zako kwenye mitandao ya kijamii, huku ukisherehekea nguvu ya mshikamano.

Jiunge na wanaharakati wengine kutoka eneo lote la kanda katika kushirikishana picha na hadithi zako pamoja nasi kwenye jukwaa hili ().

Tufuate kwenye Twitter @GBVNet, Facebook (The GBV Prevention Network), na Instagram @preventgbvnetwork, nasi tutakufuata pia! Usisahau kutushirikisha katika shughuli zako zote zinazohusiana na kampeni.

2. Vyombo vya Habari

Redio na Televisheni

Iwapo shirika lako lina uhusiano wa karibu na vyombo vya habari, televisheni na redio, unaweza kushirikiana nao ili kuandaa programu zinazoadhimisha Mshikamano wa Kifeministi na kuhamasisha uwekezaji katika kuzuia Ukatili Dhidi ya Wanawake. Unaweza kufikiria kuandaa mijadala ukishirikisha wanaharakati wa kifeministi katika jamii kama ifuatayo:

- Ni kwa namna gani umepata uzoefu wa usaidizi wa kifeministi katika maisha yako binafsi uliokusaidia kukabiliana katika kipindi kigumu?
- Ni kwa namana gani shirika lako linaweza kukuza undugu na usaidizi wa pamoja ili kukabiliana na upinzani ambao unaleta tishio katika kuzuia Ukatili Dhidi ya Wanawake na upatikanaji wa haki za kijinsia?
- Shirika lako linawezaje kuimarisha mshikamano ili kuwekeza utetezi na kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake ?
- Unawezaje kuhamasisha uwepo wa sehemu salama katika jamii yako ili kuwezesha watu kushirikishana hadithi na uzoefu wao, ili kukuza uelewa na ufahamu?

3. Taarifa kwa Vyombo vya Habari

Kuna njia kadhaa zinazoweza kukusaidia kujihusisha katika kutoa habari kwa njia ya machapisho! Tumia kutokana na mahitaji yako taarifa kwa vyombo vya habari zilizo hapo chini zifanane na muktadha wako katika ushiriki wa vyombo vya habari vya ndani na/au kuwasilisha mojawapo ya taswira za Siku 16 zinazowakilisha mshikamano/harakati za wanawake kwa magazeti/ majarida.

Kampeni za Siku 16 za Uanaharakati ya Mwaka 2023

Ikiwa ni mojawapo ya sehemu ya kampeni ya kila mwaka ya kimataifa ya kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake, Mtandao wa Kuzuia UWAKI umekuwa ukiunga mkono kampeni ya kikanda ya Siku 16 za Uanaharakati pamoja na wanachama wake kote katika Pembe ya, Mashariki na Kusini mwa Afrika tangu mwaka 2004. Katika mwaka wa 2023, lengo letu katika Siku 16 za Uanaharakati ni kujenga Mshikamano wa Kifeministi na uwekezaji katika kuzuia Ukatili Dhidi ya Wanawake.

Ukatili Dhidi ya wanawake ni tatizo la kijamii lililoenea kwa kiwango kikubwa lililoambatana na mienendo isiyo na usawa wa mamlaka kati ya wanaume na wanawake, ambayo inaimarishwa na sheria, sera, na mifumo yenye kina na kanuni za kijamii ambazo mara nyingi huwapendelea wanaume. Kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani, Mwanamke 1 kati ya 3 duniani kote wako katika hatari ya kukabiliwa na ukatili, kiwango ambacho kimedumu kwa muongo mmoja uliopita Juhudi za kushughulikia Ukatili Dhidi ya Wanawake zimeonekana kuwa za muda mrefu na ngumu kutokana na sababu nyingi, ikiwa ni pamoja na ukosefu wa ufadhili wa kutosha na ukosefu wa umakini katika kuzuia. Ni muhimu sasa kutoa wito wa kuongeza ufadhili, unaonyumbulika na wa muda mrefu ili kuwezesha uwepo wa kinga ya kimaadili yenye ufanisi katika kuzuia Ukatili Dhidi ya Wanawake.

Katika miaka ya hivi karibuni tumeshuhudia kupungua kwa nafasi ya utetezi wa kifeministi na tishio la upinzani dhidi ya haki za wanawake. Wahusika wanaopinga haki za wanawake wamezuia maendeleo, na kupunguza ufadhili kwa jumla kwenye kampeni za haki za kijinsia na kuhatarisha mfumo wa kiikolojia wa kifeministi.

Hili linahitaji hatua za pamoja, ili kuhimiza serikali kutimiza dhamira zao za kuhakikisha kunakuwa na usawa wa kijinsia, kwa kutunga sheria imara, kutenga bajeti, na kutekeleza mikakati ya kuzuia Ukatili Dhidi ya Wanawake yenye ufadhili wa kutosha na inayoendeshwa na jamii yenyewe.

Tunapoanza safari hii ya Siku 16 za Uanaharakati, tunasimama kwa umoja dhidi ya upinzani huu. Tunashirikishana uzoefu, na kuungana, na kutoa usaidizi. Tunatoa wito wa kupinga mabadiliko na kutetea uwekezaji katika kuzuia Ukatili Dhidi ya Wanawake. Jiunge nasi tunapopambana, kuungana na kuunda safu thabiti dhidi ya upinzani huu.